

SUBSIDIARY LEGISLATION

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 15 Vol. 95 dated 11th April, 2014
Printed by the Government Printer Dar es Salaam, by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 86 la tarehe 11/04/2014

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya Vifungu wa 6(1) na 16(1))

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MJI KAHAMA. ZA
MWAKA 2014

UTANGULIZI

SEHEMU YA :

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Mji wa Kahama za Mwaka 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Jina
2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Mji wa Kahama. Matumizi
3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokua pale itakapoelezwa vinginevyo:- Tafsiri
 - “Ada na Ushuru” maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri.
 - “Afisa Muidhiniwa” maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo hizi
 - “Chombo cha Usafiri” maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa mkokoteni, au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo.
 - “Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Mji wa Kahama.

Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Mji Kahama

Tangazo la Serikali Na. 86 (linaendelea)

“Kibali” maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.

“Kituo cha Mabasi” maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremsha abiria na mizigo ya Abiria.

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Kahama pamoja na Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

“Ushuru wa Matangazo” Maana yake ni ushuru machapisho, maandishi, michoro, matamshi ya aina yoyote yanayong’aa na yasiyong’aa yatolewayo na mtu yeyote. kwa madhumuni ya kuufahamisha umma juu ya upatikanaji wa huduma mbalimbali;

“Usajili, wa vyombo vya usafiri” maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

“Wakala” maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni, au asasi yoyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

SEHEMU YA II

NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Ada na
Ushuru

4.—(1) Halmashauri itatoza Ada na Ushuru mbalimbali kwa ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na Ushuru utozwayo chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla ya huduma kutolewa.

(3) Halmashauri itatenga maeneo maalumu ya kutoza Ada na Ushuru kutokana na chanzo husika.

(4) Malipo ya Ada na Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Wajibu
wa kulipa
Ada na
Ushuru

5.—(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru kuhakikisha kwamba analipa Ada na Ushuru kwa viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya utakuwa ni kuanzia saa’ kumi na mbili kamili asubuhi mpaka saa kumi na mbili jioni.

